# DOUBLE MERIT JARIBIO LA MTIHANI
# DARASA LA NANE - MWAKA 2021
# KISWAHILI
# SEHEMU YA KWANZA
# LUGHA

**2ND MERIT**

**Muda: Saa 1 Dak. 40**

## SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibu. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukishachagua jibu lionyeshe katika **KARATASI YA MA JIBU** na wala si katika kijitabu cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu: -

   **NAMBARI YAKO YA MTIHANI**

   **JINA LAKO**

   **JINA LA SHULE YAKO**
6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye nambari zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani nambari ya shule na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzoni pa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu.
9. Kwa kila swali 1-50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu MOJA tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

**Mfano:**

**Katika kijitabu cha maswali:**

**<u>Kutoka swali 16 hadi 30 chagua jibu sahihi.</u>**

**23.** Neno cherehani lina silabi ngapi?

A. 8
B. 5
C. 6
D. 4

**Jibu sahihi ni D.**

**20.** [A] [B] [C] [D]   **21.** [A] [B] [C] [D]   **22.** [A] [B] [C] [D]   **23.** [A] [B] [C] [D]

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba **23**, kisanduku chenye herufi **D** ndicho kilichochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako cheusi kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kitabu hiki cha maswali kina kurasa 8 zilizopigwa chapa.**

© Double Merit printers 2021

Email: doublemeritenterprises@gmail.com

FUNGUA KURASA

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Katika kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa .***

Ufugaji ni kazi ya ___1___ wanyama kama vile mbuzi , kondoo, ng'ombe, ngamia na wanyama wengine wengi. Wanyama hawa ___2___ kwa sababu maalum. Wapo wanyama wanotupa maziwa, nyama na ngozi. Kondoo hutupa ___3___, ___4___ hutumika ___5___ nguo. Kwato za ng'ombe hutumika kutengeneza ___6___ ilhali pembe ___7___ hutumika kutengeneza ___8___ za muziki za kupulizwa. Ngozi ___9___ mbuzi hutumiwa kutengenesa viatu. ___10___ tunayoivaa pia imetengenezwa ___11___ ngozi.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. kuwafungia | B. kuwafunga | C. kuwatunza | D. kuwatuza |
| 2. | A. hufugwa | B. hufuga | C. hufukwa | D. hufungwa |
| 3. | A. sufi | B. ngozi | C. manyoya | D. sufu |
| 4. | A. ambayo | B. ambalo | C. ambaye | D. ambazo |
| 5. | A. kutengenezea | B. kutengeza | C. kutengezea | D. kutenga |
| 6. | A. gundi | B. kundi | C. viatu | D. mikanda |
| 7. | A. zao | B. yao | C. lao | D. wao |
| 8. | A. vifaa | B. ala | C. vyombo | D. chombo |
| 9. | A. la | B. wa | C. ya | D. cha |
| 10. | A. Mkanda | B. Makoti | C. Mikanda | D. Viatu |
| 11. | A. kwa | B. na | C. mwa | D. la |

Double Merit Publishers

**Wapiga kura ___12___ maendeleo ya viongozi wao na hufanya uamuzi wa kumchagua tena au kumchagua mwengine. Kiongozi anapaswa kuwa mwadilifu. Hastahili kuwa ametajwa katika ___13___ yoyote. Apinge ___14___ kwa maneno na matendo. Ahakikishe kuwa watu ___15___ wanafurahia rasilimali za taifa kama wenzao.**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 12. | A. huchukia | B. huwasia | C. hutathmini | D. hutazama |
| 13. | A. karamu | B. kashifu | C. andamano | D. kashfa |
| 14. | A. ufisadi | B. maendeleo | C. miradi | D. uchaguzi |
| 15. | A. yake | B. wake | C. zake | D. zao |

**<u>*Kutoka swali la 16 mpaka 30, chagua jibu lililo sahihi kulingana na maagizo uliyopewa.*</u>**

16. Meli ya kivita inayoelea juu ya maji ni
   - A. merikebu
   - B. kifaru
   - C. manowari
   - D. jeti

17. Kamilisha methali ifuatayo
   Ukienda kwa mwenye chongo
   - A. funga lako jicho
   - B. kaa na yeye
   - C. mwite chongole
   - D. mwenyeji apone

18. Andika sentensi upya ukitumia ***“amba-”*** badala ya kirenjeshi ‘o’.
   Mnyama aliyechinjwa alikuwa mnono
   - A. Mnyama ambaye aliyechinjwa alikuwa mnono
   - B. Mnyama ambaye alichinjwa alikuwa mnono
   - C. Mnyama ambacho alichinjwa alikuwa mnono
   - D. Ambaye ni mnyama atachinjwa ni mnono

19. Kinyume cha shaibu ni
   - A. kijakazi
   - B. mzee
   - C. barobaro
   - D. ajuza

20. Andika kwa wingi:
   Jambo bayana halifai kubishaniwa
   - A. Majambo bayana hayafai kubishaniwa
   - B. Mambo mabayana hayafai kuyabishaniwa
   - C. Mambo bayana hayafai kubishaniwa
   - D. Mambo bayana haifai kubishaniwa

21. Maneno kama koti na korti, karamu na kalamu ni mfano wa fani gani ya lugha?
   - A. vitawe
   - B. vitate
   - C. visawe
   - D. ngeli

22. Andika tarakimu 10000009 kwa maneno.
   - A. Kumi milioni na tisa
   - B. Milioni mia moja na tisa
   - C. Elfu kumi na tisa
   - D. Milioni kumi na tisa

23. Ng'ombe saba watauzwa kesho. Saba imetumika kama

A. Kivumishi cha wingi

B. kivumishi cha msururu

C. kivumishi cha idadi kamili

D. kivumishi cha mali

24. Tegua kitendawili hiki

Nikiondoka watu hawaonani

A. upepo

B. macho

C. kivuli

D. mwangaza

25. Akisami $\frac{3}{8}$ kwa maneno ni

A. tatu kwa nane

B. thumni tatu

C. tatu nane

D. nane tatu

26. Tumia kiunganishi kinachofaa zaidi.

Wanafunzi wote wamefika ______ yeye.

A. isipokuwa

B. licha

C. lakini

D. iwapo

27. Yohana na Hamisi ni marafiki wa kufa ___

A. kufaana

B. kupona

C. kuzikana

D. kabisa

28. Tumia ***ndi-*** ya kusisitiza kujaza pengo.

Viatu vipya ______ alivyotaka sana.

A. ndio

B. ndizo

C. ndiyo

D. ndivyo

Double Merit Publishers

29. Mwalimu wetu anapenda tuwe ________

A. wasafi

B. safi

C. msafi

D. visafi

30. Kanusha:

Nimemkuta akilima vizuri

A. Amenikuta nikilima vibaya

B. Sikumkuta akilima vizuri

C. Sijamkuta akilima vizuri

D. Tumewakuta wakilima vizuri

***Soma kisa kifuatacho kisha ujibu swali 31 hadi 40.***

Kiswahili kimeenea na kuimarika humu nchini Kenya katika miongo miwili iliyopita. Kuna vyombo kadhaa ambavyo vimechangia kukua huku. Vyombo vya mawasiliano kama vile redio, runinga na magazeti vimekuwa mstari wa mbele kuchangia maenezi ya Kiswahili. Marangazo haya ya redio hufikia umma mkubwa kote nchini.

Runinga pia hutoa baadhi ya vipindi kwa Kiswahili. Taarifa ya habari ya Kiswahili huwa imeandikwa na kusomwa kwa lugha iliyoimarika sana jambo ambalo huvutia wasikilizaji na watazamaji wengi. Redio na runinga vile vile huwa na vipindi maalum vyenye lengo la kuchambua Kiswahili.

Gazeti kama vile la Taifa Leo huandikwa kwa Kiswahili na hufikia wasomaji wengi. Gazeti hili vilevile huwa na safu za lugha ya Kiswahili zenye lengo la kutoa mafunzo ya Kiswahili kwa umma angalau siku moja kwa wiki. Wataaalamu wa lugha hutoa mchango wao kuhusu masuala ya Kiswahili kupitia safu hizo.

Taasisi ya Elimu ya Kenya ni chombo kingine kilichochangia ukuaji huu wa Kiswahili. Taasisi hii hukuza mitaala inayotoa mwongozo juu ya ufundishaji wa Kiswahili nchini. Vilevile taasisi hii huchunguza vitabu vya Kiswahili vilivyochapishwa na kupendekeza vile bora vya kutumiwa shuleni.

Mashirika ya kidini hutumia lugha ya Kiswahili katika mahubiri yao. Wengine hutoa majarida yao kwa lugha hii. Shughuli za biashara na siasa zimesambaza Kiswahili kwa kuwa kama lugha ya taifa ndiyo hutumiwa katika biashara na katika mikutano ya kisiasa. Bunge pia huendesha shughuli zake kwa lugha ya Kiswahili sawa na Kiingereza. Kwa mara ya kwanza katiba imetafsiriwa kwa Kiswahili.

Kadhalika idara za Kiswahili hasa katika vyuo vikuu zimeendelea kufunza na kutayarisha walimu wa Kiswahili wanaopelekwa kufunza kote nchini idara hizi husaidia pia kusambaza msamiati mpya kupitia kwa wahadhiri.

Wataalam binafsi nao wamefanya bidii kuibua msamiati mpya hasa kutokana na teknolojia mpya na maswala mapya yanayoibuka katika jamii. Wao hutumia msamiati huo katika vitabu na hili huufanya usambae. Isitoshe, kukua na kuenea kwa Kiswahili sasa kunaelekea kupamba moto zaidi hasa kutokana na mtandao.

31. Miongo miwili ni miaka mingapi?
A. Kumi
B. Arubaini
C. Mia mbili
D. Ishirini

32. Gazeti la Taifa Leo huchangia kukua na kuenea kwa Kiswahili kwa kuwa
A. huandikwa kwa Kiswahili na lina safu kuuza lugha
B. huandikwa kwa Kiswahili na hufikia wasomaji wengi
C. hutoa mafunzo ya Kiswahili
D. huandikwa na wataalamu wengi wa lugha

33. Taasisi ya Elimu ya Kenya hufanya haya yote isipokuwa
A. kukuza mitaala
B. kuchapisha vitabu vya shule
C. kufanya utafiti
D. kupendekeza vitabu vya shule

34. Kati ya vyombo hivi, ni kipi kilicho na vituo vingi ambavyo matangazo mengi ni Kiswahili?
A. Redio
B. Runinga
C. Rununu
D. Tarakilishi

35. Miongozo juu ya kufundisha Kiswahili nchini huandaliwa na
A. vituo vya redio pekee
B. taasisi ya Elimu ya Kenya
C. wataalamu wa redio wa Taasisi ya Elimu
D. vituo vya redio na Taasisi ya Elimu

36. Lugha ya Taifa ni lugha ambayo hutumiwa
A. mikutanoni ya umma na biashara pekee
B. kuandika katiba
C. shuleni kufundishia
D. bungeni na ofisini

37. Somo la Kiswahili shuleni
A. hupendwa na waendao shuleni
B. ni la lazima na hujulikana na wote
C. ni la lazima na hutahiniwa
D. limesaidia mchango wa elimu pekee

38. Wahadhiri ni
A. waandishi
B. wataalamu
C. walimu wa chuo kikuu
D. wahazili

Double Merit Publishers

39. Kati ya msamiati ufuatao ni upi ambao umetokana na teknolojia mpya?
A. wahadhiri
B. wataalamu
C. mtandao
D. majarida

40. Kichwa mwafaka cha habari hii ni
A. Somo la Kiswahili
B. Vyombo vya Kiswahili
C. Kukua kwa lugha
D. usambazaji wa Kiswahili

***Soma kisa kifuatacho kisha ujibu swali 31 hadi 40.***

Kiswahili kimeenea na kuimarika humu nchini Kenya katika miongo miwili iliyopita. Kuna vyombo kadhaa ambavyo vimechangia kukua huku. Vyombo vya mawasiliano kama vile redio, runinga na magazeti vimekuwa mstari wa mbele kuchangia maenezi ya Kiswahili. Marangazo haya ya redio hufikia umma mkubwa kote nchini.

Runinga pia hutoa baadhi ya vipindi kwa Kiswahili. Taarifa ya habari ya Kiswahili huwa imeandikwa na kusomwa kwa lugha iliyoimarika sana jambo ambalo huvutia wasikilizaji na watazamaji wengi. Redio na runinga vile vile huwa na vipindi maalum vyenye lengo la kuchambua Kiswahili.

Gazeti kama vile la Taifa Leo huandikwa kwa Kiswahili na hufikia wasomaji wengi. Gazeti hili vilevile huwa na safu za lugha ya Kiswahili zenye lengo la kutoa mafunzo ya Kiswahili kwa umma angalau siku moja kwa wiki. Wataaalamu wa lugha hutoa mchango wao kuhusu masuala ya Kiswahili kupitia safu hizo.

Taasisi ya Elimu ya Kenya ni chombo kingine kilichochangia ukuaji huu wa Kiswahili. Taasisi hii hukuza mitaala inayotoa mwongozo juu ya ufundishaji wa Kiswahili nchini. Vilevile taasisi hii huchunguza vitabu vya Kiswahili vilivyochapishwa na kupendekeza vile bora vya kutumiwa shuleni.

Mashirika ya kidini hutumia lugha ya Kiswahili katika mahubiri yao. Wengine hutoa majarida yao kwa lugha hii. Shughuli za biashara na siasa zimesambaza Kiswahili kwa kuwa kama lugha ya taifa ndiyo hutumiwa katika biashara na katika mikutano ya kisiasa. Bunge pia huendesha shughuli zake kwa lugha ya Kiswahili sawa na Kiingereza. Kwa mara ya kwanza katiba imetafsiriwa kwa Kiswahili.

Kadhalika idara za Kiswahili hasa katika vyuo vikuu zimeendelea kufunza na kutayarisha walimu wa Kiswahili wanaopelekwa kufunza kote nchini idara hizi husaidia pia kusambaza msamiati mpya kupitia kwa wahadhiri.

Wataalam binafsi nao wamefanya bidii kuibua msamiati mpya hasa kutokana na teknolojia mpya na maswala mapya yanayoibuka katika jamii. Wao hutumia msamiati huo katika vitabu na hili huufanya usambae. Isitoshe, kukua na kuenea kwa Kiswahili sasa kunaelekea kupamba moto zaidi hasa kutokana na mtandao.

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 had 50.**

Duniani kuna aina mbalimbali za maliasili maziwa, milima, mabonde, misitu , madini, bahari, mito, visiwa, maanguko ya maji, majanga na mbuga za wanyama ni baadhi ya maliasili muhimu. Maliasili ni aali yenye manufaa katika uchumi wa nchi. Wananchi hawana budi kutunza rasilimali hizi.

Maziwa na bahari hutupatia maji mabaya hutumiwa kusafirishia shehena na pia abiria vilevile huwa na mahali pa kufanyia biashara ya kuvua samaki. Aidha maziwa na bahari huwavutia watalii wa kitaifa na wa kimataifa. Humu Afrika mna maziwa kama Viktoria, Malawi, Naivasha na Kyoga. Inadaiwa kwamba asilimia sabini na tano ya dunia imefukiwa na maji ya chumvi yaitwayo bahari. Bahari Hindi, Atlantiki na Pasifiki ndizo kubwa na maarufu ulimwenguni.

Katika ardhi kavu kuna mito chungu nzima. Mito huelekeza maji katika maziwa na pia bahari. Aghalabu mito huwa mirefu na mipana. Mito hutumika kama maskani ya wanyama wa majini na samaki mbalimbali. Maji yanayopatikana mitoni vilele hutumiwa kunyunyizia mashamba na kusafirishia mizigo kwa kweli au mashua. Mito kama vile ile, Zambezi, Kongo na Athi ni baadhi ya mito muhimu katika Afrika.

Milima na mabonde ni maliasili nyingine muhimu maishani. Milima ni miinuko ya ardhi. Kuna milima midogo na mingine mirefu kwa desturi milima mirefu huwa na theluji vileleni daima dawamu. Mlima Everest na Kilimanjaro ndiyo mirefu zaidi duniani. Mabonde kwa upande mwingine huwa mishuko mikubwa mikubwa na midogo midogo. Bonde la Ufa, Bonde la "Grand Canyon" ndiyo mabonde makuu duniani. Mabonde na milima hupamba mandhari. Pia ni mahali pa kuwavutia watalii.

Misitu aidha ni maliasili muhimu. Katika misitu kuna miti mbalimbali. Miti hutupatia mbao zinazotumiwa viwandani na katika ujenzi na utengenezaji wa samani. Misitu pia hurembesha mazingira. Inafaa wananchi waelimishwe kuhusu umuhimu wa misitu.

Maanguko ya maji ni maliasili inayovutia macho sana. Hutokea wakati mito mikubwa inapopitia kwenye mabonde makuu na mawe. Mabonde na magenge ya maji. Yanapoanguka hufanya kelele na kuonekana kama moshi. Viktoria, Chania, Nyahururu na Niagara ni miongoni mwa maanguko ya maji yanayosifika. Yafaa tuungani na tushirikiane ili kuhifadhi maliasili kama rasilimali kwa kizazi kilichoko na kijacho.

41. Ni orodha ipi ambayo ni ya maliasili?
A. Madini na bahari
B. Mabonde na madini ya chuma pekee
C. Maanguko ya maji na sehemu tambarare
D. Aali na maziwa

42. Kwa nini wananchi wanalazimika kutunza maliasili?
A. Ni muhimu katika uchumi wa nchi
B. Haina manufaa katika uchumi wa nchi
C. Hutusaidia kutunza rasilimali
D. Ni wizara yenye manufaa nchini

43. Umuhimu wa maziwa ni
A. kusafarishia shehena na ng'ombe
B. kufanyia biashara ya kuvua samaki
C. kufunika maji ya chumvi
D. kuwavutia atalii na kusafirishia shehena

44. Ni asilimia gani ya ardhi iliyofunikwa na maji ya chumvi?
A. Sabini na tatu
B. Sabini na tano
C. Sabini na nane
D. Sabini na moja

45. Bahari mbili zenye maji ya chumvi ni
A. Hindi na ziwa Naivasha
B. Atlantiki na ziwa Tanganyika
C. Atlantiki na Pasifiki
D. Pasifiki na ziwa Viktoria

46. Mito mingi huwa
A. mipana na miembamba
B. mikubwa na midogo
C. mirefu na mipana
D. mirefu na minene

47. Milima mirefu aghalabu huwa na ______ vileleni.
A. maji
B. theluji
C. moshi
D. ukungu

48. Ni milima ipi iliyo mirefu zaidi duniani?
A. Kilimanjaro na Everest
B. Everest na Kenya
C. Kilimanjaro na Elgon
D. Everest na Elgon

49. Kisawe cha <u>shehena</u> ni
A. mifuko
B. mizigo
C. uchukuzi
D. mali

50. Mwito wa mwandishi katika habari hii ni nini?
A. Kushirikiana na kukuza maliasili.
B. Kuwavutia watalii wa kitaifa na kimataifa.
C. Kuujua umuhimu wa kmalisili.
D. Tuungane na tushirikiane kuhifadhi maliasili.